[R5405]

# KILICHO HALALI SIKU YA SABATO

***LUKA 13:10-17*** ; 14: 1-6

"Sabato ilifanywa kwa ajili ya mwanadamu, na sio mwanadamu kwa ajili ya Sabato." - *MARKO 2:27*.

MKANGANYIKO mwingi umeenea kati ya Wakristo kuhusu siku ya Sabato. Chanzo kimoja cha mkanganyiko huu ni kwamba ni wachache wanaotambua kuwa mipango ya Mungu na wafuasi wa Yesu ni tofauti kabisa na ile ambayo alifanya na Israeli wa asili chini ya Agano la Sheria. Kila kitu chini ya Agano hilo kilikuwa kielelezo na kilikuwa na funzo la maana kwa Wakristo, lakini kushikilia mifano hiyo kuwa ndiyo hali halisia ni kukanganya akili zetu na kukosa uzuri na nguvu ya hali halisia.

Hakukuwa na siku ya Sabato kabla ya Sheria ya Kiyahudi, isipokuwa kwa maana kwamba neno Sabato linaashiria kupumzika, na kwamba tunaarifiwa kwamba Mungu alipumzika siku kuu ya saba, au Enzi, ya Wiki ya kazi ya Uumbaji. Henoko, ambaye alitembea na Mungu; Ibrahimu, rafiki wa Mungu, na wengine wanaompendeza Bwana, hawakujua chochote juu ya Sabato, vile tu hawakujua chochote kuhusu Siku ya Upatanisho na dhabihu zake, au mambo mengine yanayohusu Agano la Sheria la Israeli.

Mtume Paulo anaelezea kuwa Waisraeli walikuwa Nyumba ya Watumishi, chini ya Musa; lakini kwamba Kanisa ni Nyumba ya Wana, chini ya Kristo. (*Waebrania 3: 1-6*.) Njia ya Mungu ya kushughulikia Nyumba ya Watumishi itakuwa tofauti kabisa na njia Yake ya kushughulikia Nyumba ya Wana. Amri hupewa watumishi bila maelezo kwanini au mbona. Lakini Mtume anaelezea kwamba Mungu hushughulika nasi kama wana. Kwa Mkristo wa kweli, Baba wa Mbinguni hujulisha mipango Yake, madhumuni Yake, mipangilio Yake, ili wanawe, walio na Roho Wake, waweze, kwa huruma, kuingia katika mipango hiyo, kwa kutii hata kwa kiwango cha kujitolea, sio kwa sababu ya amri , lakini kwa sababu ya furaha ya kufanya mapenzi ya Baba.

Yesu na Mitume walikuwa Wayahudi, na walikuwa chini ya wajibu wa Agano la Sheria hadi wakati ambapo Yesu kwa kifo chake alikua "mwisho wa Sheria kwa haki, kwa kila mtu aaminiye." Tangu wakati huo wafuasi wa Yesu hawako chini ya neno la Sheria lililowafunga Wayahudi. Wanashughulika na Amri Kumi, kwa sababu hizo amri ndani na nje zinaonyesha mapenzi ya Mungu; na wana wote wa Mungu wanahaja ya kujua mapenzi ya Baba, ili wayaifanye kwa hiari. Lakini Mungu hasemi kwa Nyumba ya Wana, "Usiue; usiibe"; kwa maana kama wamezaliwa na Roho Mtakatifu hakika, hawatatamani kuua, wala kutaka kuiba.

Katika kushughulikia Nyumba ya Wana, Mungu, kupitia kwa Kichwa cha Nyumba, ameweka sheria mpya, ambayo ni kamili na ina maana zaidi ya ile Sheria ya Musa hapo awali ilivyoeleweka kuashiria. Ni Sheria ya Upendo. Kama vile Mtume anatangaza, "Upendo ni kutimiza Sheria." Sheria inaeleweka kwa neno moja Upendo - upendo ulio mkuu kwake Mungu, na upendo kwa wenzetu. Mwishowe, Yesu alitangaza, "Amri mpya nawapa, mpendane kama vile mimi nilivyowapenda ninyi." Alisema hivi kwetu sisi ambao tunatolea wenzetu maisha yetu.

**SIKU YA SABA — SIKU YA KWANZA**

Mapema katika kipindi cha Injili wafuasi wa Yesu walianza kukutana siku ya kwanza ya juma. Inaonekana mila hiyo ilianza kwa ukweli kwamba Yesu alifufuka kutoka kwa wafu siku hiyo,

na alionekana mara kadhaa siku hiyo kwa wafuasi Wake; na siku ya kwanza ya juma iliyofuata alijitokeza tena. Ilikuwa ni desturi kati ya wanafunzi kuwa na ushirika wao siku hiyo, sio kwamba iliagizwa na Bwana, lakini kwa sababu ya hamu yao ya kumkumbuka Mwalimu na kuwa na ushirika kati yao. Labda watunza siku ya Sabato na vilevile siku ya kwanza pia, kwa muda. Ni dhahiri walikuwa na ugumu wa kutambua jinsi walivyopita kabisa kutoka kwa utawala wa Musa na Sheria yake, na kuwa chini ya uongozi wa Yesu na mwongozo Wake - "uhuru ambako Kristo huweka huru" kabisa.

Ingawa Wakristo sasa wameacha utunzaji wa siku ya saba na kupendelea siku ya kwanza ya juma, wengi kwa makosa wanafikiria kwamba Mungu aliidhinisha mabadiliko hayo. Lakini sivyo; Mkristo hayuko chini ya sheria, lakini chini ya neema. Ilikuwa kutoka kwa upendeleo kwamba wanafunzi wa mapema walikutana pamoja siku ya kwanza, na sio kwa maagizo ya Mungu. Kwa hivyo, inapaswa kuwa bado, na ndivyo ilivyo kwa wengine. Wakristo wa kweli hawawezi kuwa na nafasi nyingi sana ya ushirika pamoja kwa ajili ya kusoma Neno la Baba wa Mbinguni, na kwa kumtolea ibada na ushirika wa mioyo yao.

Wakristo wa kweli bila shaka wanafurahi kwamba kuna siku maalum ya juma iliyotengwa, ambayo wanaweza kujitoa zaidi kwa maombi, kuabudu, kusifu na kusoma Biblia, na kufanya kazi njema — ingawa utekelezaji wa Jumapili kama hiyo umekuwa wa sheria ya kibinadamu kupitia dhana potofu. Watu wengi wa Bwana wangefurahi ikiwa mambo yao ya kidunia yangepangwa sana kiasi cha kuruhusu Jumapili mbili kwa kila wiki, au zaidi. Lakini ili kufurahiya Jumapili ipasavyo, watu wa Bwana waliojiweka wakfu wanapaswa kufunguiliwa kutoka kwa dhana potofu ambazo zinaenea sana.

**SABATO YA MAPUMZIKO**

Sheria ya Israeli ilitoa Sabato mbili. Moja, kila mwaka wa saba, iliyopata kutimizwa kwa kadiri yake kila mwaka wa hamsini, mwaka wa Yubile na mwaka wa kufunguliwa kabisa. Nyingine ilikuwa kila siku ya saba, na iliyopata hitimisho yake katika siku ya hamsini — siku ya Pentekoste — siku iliyofananisha mapumziko ambayo watu wa Mungu wanaweza kuingia hata sasa.

Mtume anarejelea haya yote mawili katika *Waebrania 4: 1-11*. Siku ya Sabato ina utimilifu wake katika mapumziko na amani ya moyo inayofurahiwa na Waisraeli wa mfano. Ni Sabato ya milele pamoja nao. Wanaingia katika pumziko. Wamefika mahali ambapo wana amani ya Mungu inayotawala mioyoni mwao. Wanapumzika kutoka kwa kazi zao wenyewe - kutoka kwa matumaini yote kwamba wangejipendekeza kwa Mungu katika kazi za aina yoyote, utunzaji wa Sabato au vinginevyo. Wanaingia katika pumziko kwa sababu wanaona kwamba Mungu amewapa katika Yesu msaada unaohitajika kwa wote, kwamba "wamekamilika katika Yeye." Pumziko hili au amani hakuna awezayekuwapokonya. Ni yao maadamu wanakaa kwa imani katika Kristo, kwa Mungu.

Lakini, kama vile Mtume anavyosema, "inabaki pumziko kwa watu wa Mungu" - pumziko la baadaye. Kanisa litaingia katika pumziko hilo wakati watapata mabadiliko yao ya ufufuo, wakati wamefanywa kama Mwokozi na kuingia kwenye furaha ya Bwana wao. Hiyo itakuwa kupumzika kamili. Kuhusu ulimwengu , Utawala mkuu wa Masihi wa miaka elfu moja itakuwa Sabato ya ulimwengu kwa jumla,

ambayo watapata fursa ya kufikia ukamilifu na kwa hivyo wataingia katika pumziko kwa kuwiana na Mungu.

Yesu alifanya miujiza yake mingi siku za Sabato, kwa upande mmoja bila shaka akisisitiza ukweli kwamba Sabato kuu, Siku ya miaka elfu moja, miaka elfu saba ya historia ya dunia, itakuwa wakati wa Ufalme Wake, ambapo wanadamu wote watapata nafasi ya kuponywa kutoka kwa dhambi na magonjwa, huzuni na maumivu, na kufikishwa katika ukamilifu kamili wa maumbile ya kibinadamu, kwa yale yote yaliyopotea katika Adamu na kukombolewa huko Kalvari.

**KUTENDA MEMA KWENYE SABATO**

Yesu kwa vile alikuwa Myahudi, alifungwa na amri zote za Sheria ya Kiyahudi, hivyo basi itakuwa kwamba hangeweza kufanya chochote kinyume na Sheria hiyo. Hakuweza kuiweka kando, na haikuwa sahihi kwamba awaeleze Wayahudi maana halisi ya Sabato. Yote ambayo yangekuja baadaye, chini ya maagizo ya Roho Mtakatifu, baada ya Pentekoste, baada ya uzawa wa Roho; kwa maana "mtu wa asili hapokei vitu vya Roho wa Mungu, wala hawezi kuvifahamu, kwa sababu vinatambuliwa kiroho." Lakini Yesu aliweza, na akafanya, kurekebisha baadhi ya kutokueleweka kwa Sheria ambayo ilikuwa imeingia kupitia mafundisho ya marabi wao, Madaktari wa Sheria, na Mafarisayo.

Hawa kwa kujionyesha walitia chumvi kwa herufi ya Sheria kwa njia nyingine, huku wakipuuza kabisa dhamira yake. Kwa hivyo wakati wanafunzi wa Yesu, walipokuwa wakipita kwenye shamba la ngano, wakisugua baadhi ya nafaka mikononi mwao ili kuzisafisha kabla ya kula, Mafarisayo walilalamika kwamba walikuwa wakivunja Sabato — walikuwa wakipura na kupepeta. Yesu alionyesha kwamba hii haikuwa sababu ya Sheria. Haikufanywa kuzuia kazi yoyote nzuri au ya lazima, bali kufaidi watu. Kulingana na Madaktari wa Sheria, kutafuta kiroboto cha kuuma itakuwa dhambi siku ya Sabato, kwa sababu itakuwa "uwindaji." Kwa hivyo kwa njia tofauti walifanya Sheria ya Mungu yenye busara ionekane kuwa isiyofaa kwa watu; na ingawa walifanya hivyo kwa upumbavu, walipuuza maswala mazito ya Sheria, ambayo yanahusu haki, upendo na rehema.

Katika somo lililo mbele yetu tuna matukio mawili ya uponyaji siku ya Sabato. Mwanamke alikuwa na ugonjwa ambao ulikuwa umemuinamisha kwa miaka kumi na nane. Yesu alimfungua kutoka utumwani mwake siku ya Sabato. Akaweka mikono yake juu yake na kusema, "Umefunguliwa kutoka kwa ungonjwa wako"; naye akanyoshwa na kumtukuza Mungu. Lakini mkuu wa sinagogi alikasirika, akawaambia watu, Kuna siku sita ambazo mnaweza kuja kuponywa, wala si siku ya Sabato.

Hii ilikusudiwa kama karipio maalum kwa Yesu, ikionyesha kwamba Yeye hakuwa mtakatifu sana na mwenye uangalifu sana juu ya Sabato kama vile alivyopaswa kuwa, lakini alikuwa mkiukaji wa Sheria. Lakini Yesu akajibu: "Enyi wanafiki! Je! Kila mmoja wenu siku ya Sabato hamfungui ng'ombe wake au punda wake katika zizi, na kumwongoza kwenda kumnywesha? , Na huyu mwanamke, aliye wa uzao wa Ibrahimu, ambaye shetani amemfunga miaka kumi na minane hii, haikumpasa afunguliwe kutoka utumwa huu siku ya Sabato? " Na maadui wake waliaibika.

Kisa kingine kilikuwa ya mtu mwenye mkono uliopooza. Yesu, akiwa anayajua mawazo yao, alishughulikia jambo hili mapema wakati huu, akiwauliza Madaktari wa Sheria na Mafarisayo, "Je! Ni

halali kuponya siku ya Sabato au la?" Hawakujibu. Kisha akamchukua yule mgonjwa, akamponya, akawauliza wakosoaji, "Ni nani kati yenu aliye na punda au ng'ombe aliyeanguka ndani ya shimo asingemvuta mara moja siku ya Sabato?" Lakini hawakuweza kujibu.

Ufahamu halisi wa Sabato, pumziko ambalo Mungu amewapa watu wake, ni baraka kubwa. "Sisi ambao tunaamini twaingia katika pumziko" - pumziko la kudumu, Sabato ya milele. Na wote kama hao wanafurahi kupata fursa maalum, kwa kadiri zinavyoweza kujitokeza, ya kukusanyika pamoja kwa jina la Bwana, katika ibada, sifa, kusoma na ushirika. Bila kujali ni siku gani, Mtume anatudokezea, Tusiache kukusanyika pamoja kama kawaida ya wengine; na zaidi, tunapoona Siku ikiwadia - Siku tukufu ya Ufalme wa Masihi inakaribia, na vivuli vya usiku na giza, vya ujinga na ushirikina vinapita. — ***Ebr . 10:25***.